



Mfuko wa Wekeza Maisha

Mfuko wa WEKEZA MAISHA ni mfuko unaoambatanisha uwekezaji pamoja na faida za bima. Zaidi ya 99% ya fedha za mwekezaji zinawekezwa na chini ya 1% zinalipia gharama za bima.

Hakuna ukomo wa kiwango cha juu cha kuwekeza isipokuwa kuna ukomo wa faida za bima ambao ni Sh. 25,000,000.

Lini nianze kuwekeza fedha zangu?

Anza kununua vipande vya Mfuko wa Wekeza Maisha mapema uwezavyo, utakavyoanza kuwekeza mapema ndivyo unapopata muda zaidi wa kuwekeza na kupata faida zaidi. Kila mwaka kiasi kitakachoongezeka (faida) kitazalisha faida nyingine katika miaka itakayofuata. Uwekezaji huu ni mfumo wa Faida Jumuishi (Compounding Interest)

Nani anaruhusiwa kuwekeza katika mfuko huu?

Mtanzania yeyote aliye na umri kati ya miaka 18-55.

Muda wa kuwekeza

Muda wa uwekezaji ni kipindi cha miaka kumi (10).

Kiasi cha kuwekeza

Kiwango cha chini cha uwekezaji kwa muda wa miaka kumi ni shilingi milioni moja (1,000,000/=) tu.

Mwekezaji ana uwezo wa kuwekeza kiasi chochote kisicho pungua shilingi 8,340/= kila mwezi.

Kwa nini Mfuko wa Wekeza Maisha?

- **Usalama:** Unaotokana na uwekezaji mseto katika hisa na dhamana mbalimbali
- **Faida:** Kuweka akiba, kukuza thamani ya fedha zako na kupata faida za bima.
- **Ukwasi:** Urahisi wa kupata sehemu au fedha zako zote pale utakapozihitaji kulingana na masharti ya mfuko.
- **Uwazi:** Thamani ya kipande inatolewa kila siku ya kazi.
- **Gharama:** Mfuko unaendeshwa kwa gharama nafuu.
- **Kuratibiwa:** Mfuko unaratibiwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana.

Faida za mfuko wa Wekeza Maisha

A. Faida za Bima

- Bima ya Maisha
- Bima ya Ajali
- Bima ya Ulemavu wa Kudumu
- Gharama ya Mazishi

B. Faida za Uwekezaji

- Ukuaji wa thamani ya uwekezaji (Vipande)
- Mkono wa pongezi baada ya uwekezaji kwa miaka kumi

Mfano:

Uwekezaji kwa kipindi cha miaka 10 katika ukuaji kati ya asilimia 8% na 15%

| Faida inayotarajiwa | 8% | 10% | 12% | 15% |
|--|-----------|--------------|--------------|--------------|
| Kiwango kilichowekezwa kwa mkupuo | 1,000,000 | 1,000,000 | 1,000,000 | 1,000,000 |
| Miaka | 10 | 10 | 10 | 10 |
| Kiwango cha awali+Riba | 1,800,000 | 2,000,000 | 2,200,000 | 2,500,000 |
| Kiwango cha awali | 2,158,925 | 2,593,742.46 | 3,105,848.21 | 4,045,557.74 |
| + riba inayokuwa/ongezeka (compound) | | | | |
| Tofauti ya faida | 358,925 | 593,742.46 | 905,848.21 | 1,545,557.74 |
| Ongezeko la kiasi kilichowekezwa miaka 10 | 2.16 | 2.59 | 3.11 | 4.05 |

Mahesabu haya yametokana na makisio ya ukuaji wa uwekezaji. Mapato ya uwekezaji yanaweza kuongezeka zaidi ya asilimia 15% au kupungua chini ya asilimia 8%.

Wekeza Kwa Njia Ya Simu

***150*82#**

KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA UTT AMIS, S.L.P 14825, GHOROFA YA PILI JENGO LA SUKARI, MATAWI YOTE YA BENKI YA CROB NCHINI • MADALALI WOTE

Simu: +255 22 2122501 | Nukushi: +255 22 2137593 | Wakala: UTT MICROFINANCE • MATAWI YOTE YA BENKI YA CROB NCHINI • MADALALI WOTE

WA SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM. | Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz | Tovuti: www.uttamis.co.tz |

Namba Za Bure +255 754 800 544 na +255 754 800 455 (VODA) +255 715 800 544 na +255 715 800 455 (TIGO) +255 782 800 455 (AIRTEL)

Tahadhari: Thamani ya kipande inaweza kuongezeka au kupungua

